JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA WAZIRI MKUU
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA WILAYA YA TANGANYIKA
SHULE YA SEKONDARI KABUNGU

Shule ya Sekondari Kabungu,

S.L.P 532
Mpanda-Katavi

10/11/2025

Namba za simu.

Mkuu wa shule: 0684341309/0756538662

Makamu Mkuu wa Shule: 0759284251/0623259351

Muhasibu wa shule: 0756950396/0623382941

Email: kabusec@gmail.com

Mzazi/Mlezi wa Mwanafunzi: ……………………………

S.L.P ………………….

## 1.0 UTANGULIZI

Ninafurahi kukutaarifu kwamba mwanao amechaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza katika shule hii mwaka 2026.

Shule ya Sekondari Kabungu ni shule ya bweni kwa wanafunzi wote wasichana na wavulana. Shule hii ipo umbali wa kilometa 8.5 Magharibi mwa makao makuu ya halmashauri ya Manispaa ya Mpanda.
Muhula wa kuanza masomo una anza tarehe 13/01/2026 na utatakiwa kuripoti shuleni kuanzia tarehe 12/01/2026 na mwisho wa kuripoti ni tarehe 27/01/2026. Ni vema kuripoti ndani ya siku kumi na nne (14)

### A. USAFIRI KUTOKA MIKOA MBALIMBALI

Kila mwanafunzi atajitegemea usafiri. Usafiri wa GARI MOSHI toka Tabora kuja Mpanda upo kila Jumatatu, Jumatano na Jumamosi, na gari moshi hufika Mpanda siku za Jumanne, Alhamisi na Jumapili.

Pia usafiri wa mabasi upo kila siku. Usafiri wa mabasi kutoka Mbeya hadi Mpanda, unapatikana kila siku kwa mabasi ya Ruchoro Express, bubele express, sadi express na ngotico express. Kutoka Arusha - Mpanda kuna mabasi ya kampuni moja tu ya uhakika ambayo ni Mumuk. Kutoka Mwanza hadi Mpanda kila siku kuna, ALLYS STAR, Esanda express, Nyehunge express na Premier line. Na kutoka Kigoma kuna mabasi ya kampuni za Adventure Connection, combas express na Superdoll.

Dar es salam kuja Mpanda kuna mabasi ya happy nation, A. N. class, na bubele logistic

Kutoka sumbawanga kuna mabasi ya princes j, ruchoro expres, na chakito express

Pia kuna usafiri wa Ndege za kampuni ya ATCL ambazo hufanya safari zake siku za Jumanne, Alhamis na Jumamosi kutoka Dar es Salaam kuja mpanda

B. USAFIRI BAADA YA KUSHUKA STENDI KUU MJINI MPANDA
usafiri wa mabasi, bajaji na pikipiki unapatikana katika kituo cha mabasi Mpanda Mjini nauli ni Tsh. 3,000/=kwa daladala na tshs 5,000/= kwa bajaji na kwa pikipiki(bodaboda) haizidi 8000/= (angalizo; *usikodi bodaboda usiku, na usije na simu eneo la shule ni kosa)*

Ni mhimu kuwasiliana kabla ya kuanza maandalizi na kabla ya kuanza safari na kama bahati mbaya simu haijapokelewa au haipatikani tuma hata ujumbe mfupi ili mhusika akiuona awasiliane nawe.

*MOTO WA SHULE: ELIMU NI KINGA*

KARIBU SANA KABUNGU SEKONDARI

ABDALLA DAWA
MKUU WA SHULE

MKUU WA SHULE
SHULE YA SEKONDARI KABUNGU
MPANDA

## 2.0. MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA

### 2.1Sare za Shule

SARE ZA DARASANI

a) Sare za shule hii ni suruali 4 (mbili) damu ya mzee na mbili khaki kwa wavulana. Na sketi 4 (mbili) damu ya mzee na mbili khaki kwa wasichana zenye kufika kwenye kifundo cha miguu na marinda madogomadogo mengi,

NB; HAIRUHUSIWI KUSHONA SKETI YA MARINDA MAKUBWA KWAKUWA SIYO SARE YETU NA HUMCHORA MTOTO. Shati ni mbili rangi nyeupe za tomato mikono mifupi, viatu vyeusi vya ngozi vya kamba.

b) Kwa wasichana wa kiislam washone nusu kanzu nyeupe na hijjab nyeupe (2).

c) T-shirt ya darasani moja rangi ya kijani yenye nembo ya shule .

d) Sweta moja rangi ya kijani ya jeshi yenye nembo ya shule

SARE ZA KUSHINDIA

a) T- shirt za kushindia mbili (2) zitakuwa ni rangi ya kijivu zenye nembo ya shule na kwa wasichana wa kiislam watashona nusu kanzu na hijab ya rangi ya kijivu 2. Aidha wasichana watashona sketi ya rangi nyeusi mbili zenye kuvuka kifundo cha mguu na wavulana watashona suruali mbili nyeusi.

b) Wasichana watavaa viatu aina ya simpo kwa ajili ya kushindia na wavulana watavaa raba rangi nyeusi.

MICHEZO

a). Sare za michezo bukta moja kwa wavulana yenye rangi nyeusi na T-shirt yenye rangi nyeusi zenye nembo.Wasichana washone sketi fupi yenye rangi ya kijani mpauko na T-shirt yenye rangi nyeusi.

(b) Viatu vya michezo, ni raba nyeupe.

SARE KWA AJILI YA MAANDALIZI YA KUSOMA USIKU

a) Mwanafunzi atavaa track suit rangi ya blue yenye mistari myeupe yenye nembo ya shule

VIFAA VYA DARASANI

(i) Daftari kubwa 13, kalamu na mkebe wa hesabu.

(ii) Taa ndogo ya sola kwa ajili ya tahadhari.

(iii) RIMU 2 (karatasi) ya A4 kwa mwaka kwa ajili ya kuandikia majaribio ya mara kwa mara.

VYOMBO VYA CHAKULA

i.Sahani (au kontena la kukingia chakula) ii.Kikombe

iii. kijiko

MALAZI KWA AJILI YA HOSTELI

I. Godoro la ukubwa wa mbili na nusu

II. Shuka 2 za rangi ya bluu bahari

III. Mto wa kulalia mmoja wenye foronya ya rangi ya shuka

IV. Blanketi 1 kwaajili ya kutumia kipindi cha baridi

MAHITAJI MENGINE

VIFAA VYA USAFI

Mwanafunzi anapokuja kuripoti aje na ndoo mbili za lita 10, jembe moja jipya lenye mpini, reki moja yenye mpini, mfagio mmoja mkubwa, mopa moja na kindoo chake, squizer moja, hard brush moja, sink brush moja na fagio la dukani moja.

MATIBABU.

01, Mwafunzi aje na tshs 50400/= kwa ajili ya bima ya afya ya NHIF.

## 3.0SHERIA NA KANUNI MUHIMU ZA SHULE HII.

Shule hii inaendeshwa kwa mujibu wa sheria ya Elimu Na.25 ya mwaka 1978 na kama ilivyorekebishwa kwa sheria Na.10 ya mwaka 1975.aidha inazingatia miongozo yote iliyotolewa na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi,yenye dhamana ya Elimu nchini na Ofisi ya Waziri mkuu-TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji Elimu.

Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yamefafanuliwa hapa.

a) Heshima kwa viongozi,wazazi,wafanyakazi wote,wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima;

b) Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule ni lazima;

c) Kushiriki kwa makini kufanya maandalio ya jioni(preparation)

d) Kuwahi katika kila shughuli za shule na nyingine utakazopewa;

e) Kufahamu mipaka ya Shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo juu ya kuwepo ndani na nje ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii;

f) Kutunza usafi wa mwili,mavazi na mazingira ya shule;

g) Kuvaa sare ya shule wakati wote ukiwa shule;

h) Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote; na

i) Kutunza mali za umma.

## 3.1MAKOSA YAFUATAYO YANAWEZA KUSABABISHA KUFUKUZWA SHULE

a. Wizi .

b. Ubakaji

c. Uasherati

d. Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevya kama vile uvutaji bangi,cocaine,mirungi,kubeli na kadhalika.

e. Kupigana au kupiga

f. Kuharibu kwa makusudi mali ya umma

g. Kudharau bendera ya Taifa

h. Kuwa mjamzito/kupata mimba

i. Kuoa au kuolewa

j. Kutoa mimba

k. Kugoma,au kuchochea na kuongoza au kushiriki kuvuruga amani na usalama wa Shule au watu.

l. Kukataa adhabu kwa makusudi.

m. Kuwa na simu ya mkononi.

n. Kumiliki kifaa chochote ambacho kinauhusiana na kuunganishwa na umeme

## MIPAKA YA SHULE

a) Mwanafunzi haruhusiwi kutembelea vijiji jirani wala kwenda mjini bila kupata kibali cha Mkuu wa Shule.
b) Mwanafunzi haruhusiwi kwenda kwenye nyumba za wafanyakazi wa shule bila idhini ya Mkuu wa Shule.
c) Mwanafunzi haruhusiwi kuonekana maeneo ya idara za masomo baada ya saa 12 jioni

1. Viambatanisho na Fomu Muhimu
   a) Fomu ya Uchunguzi wa Afya (Medical Examination Form) ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa Hospitali ya Serikali.
   b) Fomu ya maelezo binafsi kuhusu historia ya mwanafunzi/ mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai
   c) Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelekezo mengine yatakayotolewa na shule.
   d) Picha nne (4)
   e) Aje na namba mbili za simu za Wazazi na Ndugu wa karibu wa mwanafunzi wanaoweza kumtembelea mwanafunzi shuleni kwa ajili ya mawasiliano
2. Tafadhali soma kwa makini maelezo/ maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.

KARIBU SANA KATIKA SHULE HII

…………

ABDALLA K DAWA
(MKUU WA SHULE)

MKUU WA SHULE
SHULE YA SEKONDARI KABUNGU
S.L.P. 532 MPANDA

KIAMBATA ‘A`

KABUNGU SECONDARY SCHOOL,
P . O. BOX 532
MPANDA-KATAVI

FOR MEDICAL EXAMINATION

To be completed by a medical officer in respect to all form of entrants

Student’s full name

…………………………………………………………………………………….

Age ……………………………………… Years ……………………….. Sex …………………..

Blood count (red and whites)

………………………………………………………………………..

Stool examination

…………………………………………………………………………………..

Urine analysis

Syphilis and other venereal diseases test

…………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………………

T.B test

……………………………………………………………………………………………

Eye Test

…………………………………………………………………………………………….

Ears

…………………………………………………………………………………………………..

…………………………………………………………………………………………………………….

Abdomen

……………………………………………………………………………………………

Urine for plant test

…………………………………………………………………………….

ADDITIONAL INFORMATION

Defects, impotents (e.g. arms, legs etc) infections, chronic or family diseases etc

………………………………………………………………………………………………………………….

………………………………………………………………………………………………………………….

I certify that the named above is fit to pursue further studies in agricultural/domestic education

Station ………………………………………………Signature ………………………………………….

Date. …………………………………………………designation …………………………………….

KIAMBATA ‘B’

JAMUHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA WAZIRI MKUU
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA WILAYA YA TANGANYIKA
SHULE YA SEKONDARI YA KABUNGU

Kumbukumbu Namba: KBN/SS/ADI/49/2026/…………

HISTORIA YA WAZAZI NA MTOTO ALIYECHAGULIWA KUJIUNGA NA SHULE HII:-

A. WAZAZI/WALEZI

1. Jina la Baba ………………………………………………….. Hai/Si hai
2. Jina la Mama ……………………………………………….. Hai/ Si hai
3. Kama Baba si hai/ni hai jina la mlezi ni ……………………………………………………….
4. Kazi/Shughuli ya Mzazi/Mlezi …………………………………………………………..
5. Anwani ya Mzazi/Mlezi……………………………………………………………………………
6. Uraia wa wazazi
-Baba Mtanzania/Si Mtanzania
-Mama Mtanzania/ Si Mtanzania
7. Wakati wa likizo mtoto/Mwanafunzi unataka aende wapi? ……………………………………………………………………………….
8. Jina la mtu aendako ……………………………………………………..
Uhusiano na mototo/mwanafunzi.
………………………………………. ……………………………………..

SAHIHI YA BABA/MLEZI …………………………SAHIHI YA MWANAFUNZI……………………

TAREHE …………………. TAREHE ………………………….

KIAMBATA ‘C’

JAMUHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA WAZIRI MKUU
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA WILAYA YA TANGANYIKA
SHULE YA SEKONDARI KABUNGU
FORMU YA KUKUBALI KUJIUNGA NA SHULE

Mimi ……………………………………………………………………………
nimesoma kwa makini maagizo yote na ninatambua kuwa
kuchaguliwa kwangu kujiunga shule ya Sekondari kabungu ni bahati na zawadi kubwa kwa kuwa wengi wamekosa nafasi si kwa kuwa
wameshindwa ila kwa sababu ni chache.
Hivyo nakubali kujiunga na shule ya Sekondari Kabungu. Nitatii na kufuata sheria na taratibu zote za Shule.
Nitajitahidi kufanya kazi/kusoma kwa juhudi na maarifa na nitajitahidi kushirikiana na wenzangu kweli daima.
Nitalinda hadhi/heshima ya Shule na nitashirikiana na wenzangu kujenga misingi na historia nzuri ya shule.

Tarehe ………………………….. Sahihi ya mwanafunzi
………………………………………………

Mimi Mzazi/ Mlezi ………………………………………Nimeshuhudia mtoto wangu ………………………………………..
akikubali kwa hiari kujiunga na shule hiyo ninaamini mtajitahidi kumfunza na kumlea vizuri. Mimi pia naahidi kushirikiana nanyi
kikamilifu katika kumlea kijana wangu naamini tutakuwa tunawasiliana.
Tarehe ………………………………………………………………..
Sahihi ya Mzazi/Mlezi………………………………………………..